# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA

**06 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA - TAREHE 06 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**521 MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Shule za Sekondari Bulamba na Nansimo ili zitoe elimu ya Kidato cha Tano na Sita.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**522 MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali italeta Muswada wa Sheria kuhusu changomoto za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi ili ziwe kwa mujibu wa Sheria.

**WIZARA YA MAJI:**

**523 MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha mradi wa maji katika Kata ya Kalulu ili kumtua Mama ndoo kichwani na kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**524 MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini tatizo la maji litamalizwa kwa maeneo yasiyo na Mito, Mabwawa au Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria hasa Kijiji cha Kiomboi, Kitongoji cha Madole Sita.

**525 MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya changamoto ya Maji maeneo ya Jimbo la Kinondoni hususan Kata za Mwananyamala na Makumbusho.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**526 MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza migogoro ya Wafugaji na Wakulima Mkoani Morogoro.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**527 MHESHIMIWA DKT. ANGELINE SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kiwanja cha Michezo (*Centre of Excellence*) Manispaa ya Ilemela chenye hekari 16.75 ambacho kina hati tayari.

**WIZARA YA FEDHA:**

**528 MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali imepoteza fedha kiasi gani 2015 - 2020 kwa kutokuwepo usalama madhubuti wa Mifumo ya Usimamizi kufuatia mabadiliko ya TEHAMA.

**529 MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, nini mkakati wa kuyajengea uwezo Makampuni ya ndani kuyapa tenda za bilioni 50 kwani Sheria ya Manunuzi inaruhusu kupewa tenda za bilioni 20.

**530 MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali imepiga hatua gani katika kurasimisha biashara za Sekta isiyo Rasmi ili kuongeza uchumi wa nchi.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**531 MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa Wajasiriamali Wadogo ili kuwawezesha kuwa na vifungashio bora vya bidhaa zao.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**532 MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, upi mpango wa kuokoa maisha ya Wananchi kutokana na uwepo wa ajali nyingi katikati ya Mji wa Geita maeneo ya Nyankumbu na Shilabela.

**DODOMA**
**06 JUNI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**